JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# TAMKO LA SERIKALI KUHUSU MAADHIMISHO YA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI LILILOTOLEWA NA MHE. *MHANDISI.* HAMAD Y. MASAUNI (MB.), WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MUUNGANO NA MAZINGIRA, TAREHE 27 MEI, 2025

***Ndugu Wananchi,*** Kama mnavyofahamu, kila mwaka tarehe 5 Juni, nchi yetu huungana na Jumuiya ya Kimataifa kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani. Maadhimisho ya Siku ya Mazingira duniani yaliamuliwa mwaka 1972 katika mkutano wa kwanza wa Umoja wa Mataifa uliohusu masuala ya Mazingira, uliofanyika katika Mji wa Stockholm nchini Sweden.

Maadhimisho haya adhimu yaliasisiwa na nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa kwa lengo la kuelimisha wananchi kushiriki katika shughuli za hifadhi na usimamizi mazingira; kukabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira pamoja na kuhimiza matumizi endelevu ya rasilimali za mazingira duniani.

***Ndugu Wananchi,*** Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, kimataifa kwa mwaka huu yatafanyika katika **visiwa vya Jeju** nchini **Korea Kusini.** Kaulimbiu inayoongoza maadhimisho haya kimataifa kwa mwaka huu ni ***"End Plastic Pollution Globally*"** kwa Kiswahili ni ***"Komesha Uchafuzi wa Mazingira Unaochangiwa na Taka za Plastiki."*** Kaulimbiu hii inalenga kuhamasisha udhibiti wa taka zinazotokana na plastiki ambazo ni moja wapo ya changamoto kubwa ya uchafuzi wa mazingira ambao dunia inaendelea na jitihada za kutafuta ufumbuzi wake kwa kuwa na majadiliano ambayo yanalenga kuweka Mkataba wa Kimataifa wa kudhibiti Plastiki ambapo Mkutano wa majadiliano wa suala hili utafanyika nchini Korea.

Aidha, kama ilivyo kawaida yetu nchini, mbali na kuwa na kaulimbiu ya Kimataifa, nchi yetu imekuwa na utaratibu wa kuwa na kaulimbiu ya kitaifa kuendana na muktadha wa masuala ya hifadhi ya mazingira nchini kwa kuzingatia changamoto, mahitaji na fursa mbalimbali zilizopo nchini zinazohusu hifadhi ya mazingira. Kwa muktadha huu, Maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Mazingira Duniani yatafanyika katika Jiji la Dodoma na yataongozwa na kaulimbiu inayosema: "***Mazingira Yetu na Tanzania Ijayo Tuwajibike Sasa, Dhibiti Matumizi ya Plastiki."***

***Ndugu Wananchi,*** Kauli mbiu hii inalenga kuikumbusha jamii yetu ya Tanzania kuwa mazingira na rasilimali zake ni msingi wa uhai na maisha yetu pamoja na ukuaji wa uchumi. Hivyo utunzaji na uhifadhi wa mazingira na rasilimali zake ni jambo muhimu kwa kila mmoja wetu.

Naomba niwakumbushe kuwa Tanzania yetu tuliyoipokea kwa mababu zetu hatuna budi kuitunza kwa kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali zake ili kama tulivyorithishwa na mababu zetu pia tuirithishe kwa vizazi vijavyo ili navyo viweze kupata mahitaji yake ya kijamii na kiuchumi.

***Ndugu Wananchi,***

Mnamo tarehe 9 Aprili, 2019 Serikali ilitoa tamko la kusitisha Uzalishaji; Uingizaji nchini, Usafirishaji nje ya nchi; Usambazaji; na Matumizi ya mifuko ya plastiki nchini kuanzia tarehe 1 Juni, 2019. Mara baada ya agizo hilo Serikali iliandaa Kanuni zilizochapishwa katika Gazeti la Serikali Na. 394 tarehe 17/5/2019. Kanuni hizi ni za Usimamizi wa Mazingira za Kupiga Marufuku Mifuko ya Plastiki za Mwaka 2019. Aidha, mnamo mwaka 2022, Kanuni husika zilifanyiwa mapitio na kuwa na Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Kupiga Marufuku Mifuko ya Plastiki na Lakiri za Vifuniko vya Plastiki) za Mwaka, 2022. Kanuni hizi zilifuta Kanuni za mwaka 2019.

Kwa kiasi kikubwa nchi yetu imepiga hatua katika kudhibiti taka za plastiki baada ya kupiga marufuku uzalishaji, uingizaji, usambazaji na matumizi ya mifuko ya plastiki kuanzia Juni, 2019. Hii, ilisaidia kupunguza uchafuzi wa mazingira, kuboresha taswira za miji na kuhamasisha matumizi ya mifuko mbadala. Katazo hili limeendana na elimu kwa umma sambamba na ushirikishwaji wa sekta binafsi katika uzalishaji wa mifuko mbadala ambazo ni rafiki kwa mazingira.

***Ndugu Wananchi,*** mtakubaliana na mimi kuwa pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kusimamia utekelezaji wa marufuku husika, siku za hivi karibuni kumejitokeza changamoto ya matumizi ya vifungashio vya plastiki aina ya *tubings* kutumika kama vibebeo na vifungashio hivyo havina sifa na hivyo kutokukidhi matakwa yaliyowekwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Naomba kutumia fursa hii kutoa onyo kali kwa watu na makampuni ambayo yanaendelea kuzalisha bidhaa za mifuko ya plastiki ambayo imepigwa marufuku na kuingiza katika matumizi kwa njia za panya. Serikali itaendelea kufanya doria za kushtukiza katika viwanda, viwanda bubu na masoko ili kuwabaini na kuwachukulia hatua wote wanaojihusisha na biashara hii haramu.

Pia natoa maelekezo kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mamlaka nyingine za umma kuendeleza juhudi za kufuatilia na kubaini ukiukwaji wa Sheria unaohusisha uzalishaji wa bidhaa za plastiki zilizopigwa marufuku kuzalishwa na kutumika nchini. Natoa wito kwa kuwakumbusha watanzania wenzangu, kuzingatia maelekezo ya Serikali kuachana na mifuko ya plastiki na kutumia mifuko mbadala ambayo kwa sasa inapatikana nchini kote kwa gharama nafuu.

***Ndugu Wananchi,*** kama nilivyoeleza hapo awali kuwa kwa mwaka huu 2025 Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yatafanyika katika Jiji la Dodoma na shughuli za maadhimisho zitaanza rasmi tarehe 01 Juni hadi 5 Juni, 2025. Shughuli zilizopangwa kufanyika wakati wa maadhimisho hayo ni kama ifuatavyo:

i. Kutakuwa na Mkutano wa Vijana (*Youth Summit)* ambao utakutanisha pamoja vijana mbalimbali ikiwemo wanafunzi wa vyuo, wajasiriamali na mabalozi wa mazingira ambao wanajishughulisha na masuala ya hifadhi ya Mazingira. Katika mkutano huo kutafanyika Uzinduzi wa Mkakati wa Usimamizi wa Taka.

ii. **Tarehe 5 Juni, 2025,** itakuwa ndio siku ya kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani ambapo Mgeni Rasmi wa hafla hiyo anatarajiwa kuwa ***Mheshimiwa*** **Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** Katika hafla hiyo mgeni rasmi atahutubia Viongozi wa Serikali pamoja na wananchi wa Jiji la Dodoma pamoja na wananchi wote kupitia vyombo vya habari. Shughuli nyingine zotakazofanyika siku ya kilele ni pamoja na:

   i. Uzinduzi wa Taarifa ya Nne ya Hali ya Mazingira nchini

   ii. Uzinduzi wa Mfumo wa kuwasilisha Taarifa za Mazingira kutoka kwa wadau;

   iii. Utoaji wa Tuzo ya Nishati safi ya kupikia kwa Taasisi zinazolisha watu zaidi ya 100 kwa siku; na

   iv. Tuzo za utunzaji bora wa Bustani za Kijani katika Miji na Majiji.

***Ndugu wananchi,***

Kabla ya kuhitimisha Tamko langu, Napenda kuwashukuru wadau wote wa Mazingira na Washirika wa Maendeleo kwa kuendelea kushirikiana na Serikali ikiwemo Ofisi ya Makamu wa Rais katika kutekeleza shughuli na miradi mbalimbali ya kuhifadhi mazingira. Ni matumami yangu kuwa tutaendelea kushirikiana kwa karibu zaidi ili kukabiliana na changamoto za hifadhi ya mazingira na kuleta maendeleo endelevu nchini.

Napenda pia kuchukua fursa hii kuwashukuru vyombo vya habari kwa kutumia muda wao kuhamasisha jamii kwenye masuala ya hifadhi ya mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali zake. Aidha, nizishukuru taasisi zote za Serikali, asasi za kiraia na asasi

za kimataifa kwa kushirikiana na Serikali katika jitihada mbalimbali za kupambana na uharibifu wa mazingira.

***Ndugu Wananchi,*** Mwisho, natoa wito kwa Mikoa yote kutumia radio za kijamii zilizopo katika Halmashauri na Mikoa yenu kuhamasishana na kuelimisha jamii kwenye masuala yahusuyo hifadhi ya mazingira ikiwemo kutumia nishati mbadala wa mkaa, majiko banifu pamoja na kutumia njia sahihi za kuhifadhi taka. Tukumbuke kwamba, suala la hifadhi ya mazingira ni jukumu letu sote na tunapaswa kulitekeleza kwa vitendo.

"***Mazingira Yetu na Tanzania Ijayo Tuwajibike Sasa, Dhibiti Matumizi ya Plastiki.***"

*Mhandisi* Hamad M.Y Masauni (Mb.),

**WAZIRI WA NCHI - OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

**(MUUNGANO NA MAZINGIRA)**